TAMKO KUHUSU NIA YA TANZANIA KUJITOA KWENYE AZIMIO LINALORUHUSU WANANCHI NA ASASI ZA KIRAIA KUPELEKA MALALAMIKO MOJA KWA MOJA KATIKA MAHAKAMA YA AFRIKA YA HAKI ZA BINADAMU NA WATU

1.0 Utangulizi

Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC) pamoja na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) tumepokea kwa masikitiko kitendo cha Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kujitoa katika Azimio (declaration) linaloruhusu Wananchi pamoja na Asasi zisizo za Kiserikali kupeleka malalamiko moja kwa moja mbele ya Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu.

Kwa mujibu wa Notisi/Taarifa iliyotolewa na kusainiwa na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Profesa Palamagamba Kabudi, Tanzania imeamua kujitoa katika Azimio iliyokuwa imeweka kutokana na Azimio hilo kutumika kinyume na mambo ambayo Tanzania iliyawekea mipaka (reservations). Hata hivyo, kwa mujibu wa Azimio lililowekwa na Tanzania katika Mahakama ya Afrika, masharti pekee yaliyowekwa na Tanzania yalilenga kuhakikisha watu binafsi na mashirika wanapitia mifumo yote ya ndani kabla ya kupeleka kesi katika mahakama hiyo.

Azimio hili limekuwa likifuatwa na hata pale walalamikaji wanapokiuka, mawakili wa serikali wamekuwa wakiweka pingamizi kwa mashauri hayo. Hivyo tunaamini sababu hii pekee haitoshi kupelekea Serikali kujitoa. Ikumbukwe kwamba mnamo Novemba 22, 2019, Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu ilitoa taarifa inayoonesha kudorora kwa hali ya haki za binadamu Tanzania hivyo kujitoa kwa Tanzania kunaweza kuleta picha ya kukwepa kuboresha hali ya haki za binadamu.

Taarifa za Tanzania kujitoa zimethibitishwa pia na Waziri wa Katiba na Sheria, Balozi Augustino Mahiga ambaye alisisitiza kuwa Tanzania haijajitoa kuendelea kufanya kazi na Mahakama ya Afrika bali imejitoa kwenye Azimio lake la kuruhusu Wananchi na Asasi za Kiraia kupeleka malalamiko yao moja kwa moja katika Mahakama ya Afrika. Watetezi TV walipomuhoji Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Profesa Kabudi alieleza kwamba taarifa/ufafanuzi uliotolewa na Waziri wa Katiba na Sheria na sahihi na huo ndio msimamo kwa sasa.

Ikumbukwe kuwa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu imeanzishwa kwa mujibu wa Ibara ya 1 ya Mkataba ya Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu.

Kuanzishwa kwa mahakama hiyo ni muendelezo wa juhudi za ulinzi na utetezi wa haki za binadamu unaofanywa na Kamisheni ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu. Mahakama hiyo ina makao makuu yake jijini Arusha nchini Tanzania.

2.0 Kuhusu Azimio la Kuruhusu Wananchi na AZAKI kupeleka malalamiko moja kwa moja katika mahakama ya Afrika.

Ibara ya 34 (6) ya Mkataba unaoanzisha Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu inaeleza bayana kuwa; Muda wowote baada ya nchi kuridhia Mkataba inaweza kutoa Azimio la kukubali Mahakama kupokea malalamiko (kesi) kwa mujibu wa Ibara ya 5(3) ya Mkataba. Na kwa maana hiyo Mahakama haitakuwa na uwezo wa kusikiliza malalamiko/kesi itakayoletwa kwa mujibu wa Ibara ya 5(3) endapo kesi hiyo inaihusu nchi ambayo haijaweka Azimio.

Ibara ya 5(3) inasema Mahakama inaweza kuruhusu Asasi za Kiraia zenye hadhi ya uangalizi (Observer Status) mbele ya Kamisheni ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu pamoja na wananchi kupeleka maombi mbele ya mahakama hiyo kwa mujibu wa Ibara ya 34(6) ya Mkataba.

Mkataba unaoanzisha Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu haijaweka ukomo wa muda ambao nchi mwanachama inaweza kujitoa katika Azimio lililoweka. Hata hivyo Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu ililiangazia suala hili katika kesi ya Ingabire Victoire Umuhoza dhidi ya Rwanda ambapo moja ya masuala yaliyojadiliwa katika kesi hii ni mamlaka ya mahakama kusikiliza zinazohusu nchi kujitoa kwenye Azimio lililowekwa, uhalali wa nchi kujitoa, madhara ya nchi kujitoa na umuhimu wa kutoa taarifa/notisi ya kujitoa. Katika maamuzi yake juu ya muda wa notisi ya kujitoa katika muda maalumu.

Katika kutoa uamuzi wake juu ya umuhimu wa taarifa na muda wa utoaji wa notisi, Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu ilitolea mifano ya Mkataba wa Amerika wa Haki za Binadamu pamoja na kifungu cha 56 (2) cha Mkataba wa Vienna ambapo masharti ya kujitoa ni lazima nchi itoe Notisi ya mwaka mmoja. Hivyo, kwa kuzingatia Notisi iliyosainiwa na Waziri wa Mambo ya Nje na Uhusiano wa Afrika Mashariki, Profesa Palamagamba John Kabudi, iliyosainiwa tarehe 14 Novemba, 2019, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania sasa itahesabika kwamba imejitoa rasmi mnamo tarehe 14 mwezi Novemba mwaka 2020 ambapo ndipo kipindi cha notisi ya mwaka mmoja kitakuwa kimeisha. Pia katika kesi tajwa hapo juu, mahakama ilieleza kwamba, itaendelea kuwa na mamlaka ya kusikiliza na kumaliza kesi zote ambazo hazijamalizika kwakuwa sheria inaenda mbele na hairudi nyuma (the principle legal-retroactivity). Hivyo, mashauri yote yaliyoko katika mahakama hiyo yataendelea kusikilizwa hadi yatolewe maamuzi.

3.0 Sababu za Tanzania Kujitoa

Kama ilivyoelezwa hapo mwanzo, Tanzania imejitoa katika Azimio lake la kuruhusu wananchi na AZAKI kuilalamikia Mahakama ya Afrika kwa kile kilichodaiwa kwamba Azimio hilo limekuwa likitumika kinyume na mipaka (reservations) ambayo Tanzania illiweka wakati wa

kusaini Mkataba. Hata hivyo, wanufaika wa Azimio hilo hawajaweza kushirikishwa kabla ya maamuzi kujitoa kutolewa. **Kujitoa bila kushirikisha wadau/wanufaika wa Azimio kumezua sintofahamu ukizingatia pia kuwa, mipaka iliyowekwa imekuwa ikizingatiwa na wadau na hivyo kushindwa kuelewa ni sababu ipi haswa imesababisha nchi yetu kujitoa**. Pia, haijulikani ni kwa namna gani serikali iliwahusisha wadau katika meza ya majadiliano ili kuweza kurekebisha kasoro ambazo zimekuwa zikisababisha ukiukwaji wa mipaka iliyowekwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati inatia sahihi Mkataba unaoanzisha mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu. Tunaamini, serikali ingewashirikisha wadau, tungeweza kuwa na suluhisho bora zaidi kuliko kujitoa.

4.0 Historia ya Nchi kujitoa katika Azimio la kuruhusu Raia na AZAKI kuilalamikia mahakama ya Afrika

Tanzania inakuwa ni nchi ya pili kujitoa baada ya Rwanda ambayo ilijitoa 29 February mwaka 2016. Historia inaonyesha kwamba, nchi zinazojitoa katika Azimio hilo zimekuwa zikilalamikiwa sana katika Mahakama ya Afrika kutokana na hali ya ukiukwaji wa Haki za Binadamu katika nchi hizo. Mpaka sasa, zipo kesi 70 kutoka Tanzania za mashirika na watu binafsi ambazo hazijaisha katika Mahakama hiyo.

Pia katika kesi 62 zilizowahi kutolewa maamuzi na mahakama ya Afrika kesi 32 ni za Tanzania na zilifunguliwa na Mashirika na Watu binafsi dhidi ya Serikali ya Tanzania. Tanzania inafuatiwa na Rwanda ambyo katika mashauri 62 yaliyowahi kutolewa maamuzi na mahakama ya Afrika mashauri 10 ni kutoka Rwanda (kwa taarifa zaidi http://en.african-court.org/index.php/cases/2016-10-17-16-18-21#finalised-cases). Aidha, katika Mashauri 172 ambayo hayajaisha mahakamani hapo, mashauri 105 ni kutoka Tanzania ambapo mashauri 70 yalifunguliwa na AZAKI na raia wa Tanzania na mashauri 33 yamefunguliwa na nchi, taasisi na raia wa nchi nyingine dhidi ya Tanzania (kwa taarifa Zaidi za kesi hizo tembelea http://en.african-court.org/index.php/cases/2016-10-17-16-18-21#pending-cases). Hii inaonyesha dhahiri ni jinsi gani Tanzania imekuwa ikilalamikiwa katika uvunjifu wa Haki za Binadamu. Pia tamko la Kamisheni ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu kuhusu mdororo wa hali ya Haki za Binadamu nchini ni kiashiria kingine kinachoonyesha hali ya ukiukwaji wa Haki za binadamu nchini.

Historia pia inaonyesha kuwa, Tanzania imekuwa ikipuuzia maamuzi halali ambayo yamekuwa yakitolewa na Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu na hivyo kuzua maswali kama kweli nchi yetu imeridhia Mkataba inayoanzisha mahakama hiyo kwa nia njema (in good faith). Baadhi ya Maamuzi yaliyowahi kutolewa na Mahakama hiyo hadi leo hii hayajatekelezwa ni pamoja na Kesi ya Mgombea Binafsi iliyofunguliwa na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu, Tanganyika Law Society na Marehemu Christopher Mtikila, Kesi ya Kupinga Adhabu ya Kifo pamoja na kesi nyingine nyingi (kwa taarifa Zaidi tembelea http://en.african-court.org/index.php/cases/2016-10-17-16-18-21#finalised-cases)

5.0 Madhara ya Kujitoa

Mbali na kwamba, wananchi na Asasi za Kiraia Tanzania kwa sasa watakuwa hawana uwezo wa kupeleka malalamiko yao moja kwa moja mbele ya Mahakama, kutakuwa na kero na mlolongo mkubwa wa kuifikia Mahakama hiyo kwakuwa sasa inabidi raia au Asasi kuifikia mahakama hiyo kupitia Kamisheni ya Haki za Binadamu na Watu ambayo ina makao yake makuu Banjul nchini Gambia.

Wananchi watakosa haki ya kukata rufaa baada ya kushindwa kupata haki katika mahakama za ndani.

Pia, kujitoa kwa Tanzania kunaleta taswira mbaya kitaifa na kimataifa ukizingatia kwamba sisi ndio wenyeji wa Mahakama hiyo na hivyo tulitakiwa tuwe mfano wa kuigwa. Ni dhahiri pia kwamba, ukiukwaji wa haki za binadamu uliokuwa ukiendelea nchini unaweza kuongezeka haswa ukizingatia kwamba wananchi na AZAKi wamenyimwa fursa ya kuifikia mahakama hiyo kwa njia rahisi na nafuu kwani mahakama hiyo iko hapa hapa nchini.

Kwa mujibu wa takwimu kesi nyingi zilizopo mahakamani hapo zimefunguliwa na watanzania na hii ni kwa sababu ya urahisi kwa Watanzania kufikia mahakama hiyo. Kujitoa kwa Tanzania itapelekea mahakama hiyo kutokuwa na mashauri ya kutosha na hivyo kusababisha rasilimali kutumika bila kuwanufaisha Watanzania.

6.0 Wito Wetu

1. Tunaiomba Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ifikirie upya uamuzi wake wa kujitoa na ikiwezekana ibadilishe maamuzi kwani msimamo wa kujitoa unaleta taswira mbaya na unawanyima wananchi na AZAKI fursa ya kuifikia mahakama hiyo kupata haki zao kwa urahisi na unafuu.
2. Serikali iwahusishe wadau katika meza ya majadiliano ili kutatua kwa pamoja changamoto zilizojitokeza na kupelekea ukiukwaji wa mipaka iliyowekwa na serikali (kama ipo) wakati wa kuruhusu Azimio la kuruhusu wananchi na AZAKI kuilalamikia mahakama moja kwa moja.
3. Tunaisihi Serikali itekeleze maamuzi ya mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu kwa nia njema ili iendelee kuhifadhi taswira ya nchi mwenyeji wa mahakama hiyo.

4. Tunaziomba Asasi za Kiraia pamoja na wananchi kuendelea kutumia Kamisheni ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu pamoja na Mahakama ya Afrika Mashariki kupeleka malalamiko yao pale wanapoona haki zao zinavunjwa. Pia watumie kipindi hiki cha mwaka mmoja ambapo Tanzania imetoa Notisi kuweza kudai haki zao katika Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu.
5. Sisi kama Asasi za Kiraia tunaona ni wakati sasa Umoja wa Afrika (AU) kufikiria kuondoa takwa la nchi kuwa na hiari ya kujiwekea Azimio la kuruhusu wananchi na AZAKI kupeleka malalamiko mbele ya Mahakama ya Afrika kwakuwa suala hilo linawanyima haki wananchi wan chi za Afrika kudai haki zao katika mahakama iliyoundwa kwa ajili yao.

Imetolewa leo tarehe 4.12.2019
Na

……
Onesmo Olengurumwa,
Mratibu Kitaifa, Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC) pamoja na

…….
Anna Aloyce Henga
Mkurugenzi Mtendaji, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC)